# Nafasi ya Mwanamke Mgodini: Mapambano na Matumaini ya Wanawake Katika Sekta ya Madini ya Vito Kalalani, Tanga

Haki Madini
Septemba 2025

## Muhtasari


Katika Tanzania, sekta ya madini ina mchango mkubwa katika uchumi wa taifa na katika kuboresha maisha ya watu, hasa katika maeneo ya vijijini yenye rasilimali za asili. Hata hivyo, ushiriki katika sekta hii umeendelea kuwa wa kijinsia, ambapo wanawake wamekuwa wakitengwa katika maamuzi na hawawakilishwi vya kutosha katika nafasi zenye faida kubwa, hususan katika sekta ndogo ya madini ya vito. Eneo la machimbo ya vito katika kata ya Kalalani, wilayani Korogwe mkoa wa Tanga, ni mfano mzuri wa kuchambua ushiriki wa wanawake katika sekta hii inayotawaliwa na wanaume, pamoja na changamoto na fursa zilizopo kwa ajili ya maendeleo jumuishi.

Utafiti huu umefanyika kwa lengo la kubaini na kuchambua vikwazo vinavyokwamisha ushiriki wa wanawake katika sekta ya madini ya vito Kalalani. Pia utafiti huu unalenga kuainisha fursa zilizopo na kupendekeza mikakati madhubuti ya kuongeza ushiriki wao. Utafiti huu ni wa wakati muafaka, hasa ikizingatiwa kuwa jamii nyingi za vijijini zinazidi kuwa hatarini kiuchumi kutokana na kushuka kwa kilimo – ambacho ndicho chanzo kikuu cha mapato – kwa sababu ya ukame wa muda mrefu na mabadiliko ya tabianchi. Katika muktadha huu, sekta ya madini ya vito inatoa fursa mbadala au ya ziada ya kipato kwa wanawake.

Utafiti umejikita katika maswali matatu ya msingi:

1. Ni vikwazo gani vinavyokwamisha ushiriki kamili wa wanawake katika sekta ya madini ya vito ya Kalalani?

2. Ni fursa gani zilizopo ambazo zinaweza kusaidia kuimarisha ushiriki wa wanawake?

3. Ni mikakati gani inayoweza kutekelezwa na wadau ili kuboresha ushiriki wa wanawake katika uchimbaji na biashara ya madini ya vito?

Utafiti ulitumia mbinu ya kidadisi, ikiwa ni pamoja na majadiliano ya vikund, mahojiano na wadau muhimu, na uchunguzi wa moja kwa moja. Waliohojiwa walijumuisha wanawake wachimbaji, maafisa wa serikali za mitaa, viongozi wa jamii na wadau wengine wa sekta ya madini ya vito. Utafiti ulifanyika katika kata ya Kalalani na vijiji vinavyoizunguka ndani ya wilaya ya Korogwe.

Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa wanawake wanakabiliwa na vikwazo vingi vya kimfumo na vya kijamii, ikiwa ni pamoja na mila na desturi kandamizi zinazowakatisha tamaa kujiingiza katika shughuli za madini, ukosefu wa mitaji na vifaa, ujuzi mdogo wa kiufundi, na kutengwa katika umiliki wa ardhi na majukwaa ya maamuzi. Aidha, wanawake wengi hawana fursa ya kupata leseni za madini na hukabiliwa na hatari za kiafya kazini bila vifaa vya kujikinga au huduma bora za afya. Uharibifu wa mazingira unaosababishwa na shughuli holela za uchimbaji pia huwaathiri zaidi wanawake, hasa wale wanaotegemea kilimo na vyanzo vya maji vilivyo karibu na migodi.

Pamoja na changamoto hizo, utafiti ulibaini kuwa kuna fursa kadhaa zinazoweza kutumika kuinua ushiriki wa wanawake katika sekta hii. Fursa hizo ni pamoja na ajira katika shughuli zinazohusiana na uchimbaji kama vile kuchambua, kusaga na kusafisha vito, pamoja na shughuli zisizo za uchimbaji kama vile uuzaji wa chakula na huduma nyingine za kusaidia katika maeneo ya migodi. Vilevile, uwepo wa mifumo ya kisheria na sera za kitaifa, ikiwemo Sheria ya Madini na sera za jinsia, vinatoa msingi wa kuandaa afua mahsusi kwa wanawake. Aidha, baadhi ya wanawake walionyesha nia ya kuunda vikundi au vyama vya ushirika ili kuongeza sauti na nguvu ya pamoja.

Hata hivyo, utafiti pia ulibaini kuwa utekelezaji wa sera hizi katika ngazi ya mtaa ni dhaifu, na wanawake wengi hawana uelewa wa kutosha juu ya sera na sheria zilizopo. Ukosefu wa programu endelevu za kujenga uwezo na kuwafikia wanawake pia unaendeleza hali ya kutengwa kwao katika kunufaika na sekta ya madini.

Kwa ujumla, ingawa sekta ya madini ya vito Kalalani inatoa fursa za kiuchumi moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja kwa wanawake, ushiriki wao bado ni mdogo kutokana na vikwazo vya kisheria, kijamii na kiuchumi. Kukabiliana na changamoto hizi kunahitaji ushirikiano wa karibu kati ya wadau, utekelezaji wa makusudi wa sera zilizopo, na kuhusisha jamii kwa njia endelevu ili kukuza maendeleo jumuishi na yenye usawa wa kijinsia.

**Mapendekezo muhimu ni pamoja na:**

- Kuelimisha wanawake kuhusu haki na fursa zao za kisheria kupitia programu maalum za elimu na kujenga wa uwezo.
- Kusaidia uundwaji wa vikundi vya wanawake na vyama vya ushirika ili kuongeza ushawishi wao wa pamoja.
- Kusimamia utekelezaji wa sheria zinazohimiza usawa wa kijinsia katika utoaji wa leseni, ajira, na mgawanyo wa rasilimali.
- Kujumuisha bajeti na mipango jumuishi ya kijinsia katika mipango ya maendeleo ya serikali za mitaa.
- Kuboresha viwango vya afya na usalama kwa wanawake wanaofanya kazi migodini na maeneo yanayozunguka migodi.
- Kuwezesha upatikanaji wa mitaji, teknolojia, na mafunzo kwa wanawake ili washiriki katika shughuli zenye thamani ya juu katika mnyororo wa madini ya vito.

Chapisho hili ni sehemu ya mfululizo wa "Sauti za Watanzania" wa IPIS na toleo lake kuhusu *"Ushiriki na ujumuishwaji wa wanawake katika sekta ya uziduaji Tanzania"*

Ripoti kamili ya kifani hii inapatikana kwa Kiingereza kupitia: https://ipisresearch.be/home/capacity-enhancement/voices-from-the-south/voices-from-tanzania/

mawasiliano
info@hakimadini.org

Belgium partner in development

Kwa msaada wa IPIS